**MASHARTI YA JUMLA KWA MADEREVA**
Maboresho ya 17 Oktoba 2024

**Unaweza kupakua nakala ya nje ya mtandao ya masharti haya kwa ajili ya kumbukumbu zako na matumizi ya baadae hapa.**

Masharti haya ya Jumla yanaweka vigezo na masharti muhimu yanayotumika na kutawala/kuongoza matumizi ya huduma za Bolt. Ili kutoa Huduma za Usafiri kupitia Jukwaa la Bolt, unapaswa kukubaliana na Vigezo na Masharti kama yalivyoainishwa hapa chini.

1. **MAANA**
2.
    1. **Bolt** (ambayo pia itajulikana kama "sisi" au "wetu") - **Bolt Operations OÜ ni kampuni binafsi iliyoundwa na kusajiliwa kwa sheria za Jamhuri ya Estonia yenye alama ya usajili 14532901, na ofisi zilizosajiliwa zikiwa Vana-Luona tn 15, Tallinn 10134, Jamhuri ya Estonia, pia kundi la makapuni ya Bolt na Washirika.** Kundi la Bolt litamaanisha makampuni makampuni ambayo Bolt Operations OÜ inayasimamia (mfano makampuni tanzu ya Bolt Operations OÜ). Washirika wa Bolt itamaanisha wawakilishi wa ndani, washirika, mawakala walioteuliwa na Bolt Operations OÜ. Orodha ya kundi la makampuni ya Bolt na washirika inapatikana katika tovuti https://bolt.eu/cities/.
    2. **Huduma za Bolt –** huduma zitolewazo na Bolt, ikiwemo utoaji na matengenezo ya programu ya Bolt, jukwaa la Bolt, malipo ya kimfumo, msaada kwa mteja, mawasiliano kati ya Dereva na abiria na huduma nyingine zinazoendana.
    3. **Programu ya Bolt –** ni programu ya simu kwa ajili ya Madereva na Wasafiri kuomba na kupata huduma za Usafiri.
    4. **Jukwaa la Bolt –** ni teknolojia inayowaunganisha Abiria na Madereva kuwasaidia kuzunguka mjini kwa ufanisi zaidi.
    5. **Abiria** – ni mtu anayeomba huduma za usafiri kwa kutumia mfumo wa Bolt.
    6. **Dereva** (pia ikimaanisha "wewe") – ni mtu anayetoa huduma za usafiri kupitia programu ya Bolt. Kila dereva atapata akaunti yake binafsi ya Dereva wa Bolt kwa ajili ya kutumia kwenye programu ya Bolt na jukwaa la Bolt.
    7. **Makubaliano –** haya ni makubaliano kati ya Dereva na Bolt kuhusiana na matumizi ya huduma za Bolt inayohusisha mambo yafuatayo:
    8.
        1. Masharti haya ya jumla;
        2. Masharti maalumu yanayooneshwa kwenye programu ya Bolt, mfano kuhusu taarifa za nauli au maelezo ya huduma;
        3. Masharti mengine yanayotumika kwenye huduma za Bolt ikiwa ni pamoja na masharti na sera kwa ajili ya tukio husika, shughuli au matangazo;
        4. miongozo kwa Madereva; na
        5. Masharti mengine yaliyoainishwa katika Makubaliano haya kadri yatakavyorekebishwa mara kwa mara.
    9. **Nauli** – ni ada anayopaswa kulipa abiria kwa dereva kwa ajili ya huduma za usafiri.
    10. **Ada ya Bolt** – ada inayopaswa kulipwa na dereva kwa Bolt kwa ajili ya kutumia jukwaa la Bolt.
    11. **Malipo ndani ya programu** – kadi, gharama za ubebaji na njia nyingine za kimalipo zinazotumiwa na Mteja kupitia mfumo wa Bolt kwa ajili ya Huduma za Usafiri.

12. **Akaunti ya Dereva wa Bolt** – njia ya kufikia tovuti yenye taarifa na nyaraka zinazohusu matumizi ya huduma za Bolt wakati wa kutoa huduma za Usafiri, ikiwemo nyaraka za uhasibu. Dereva anaweza kufikia Akaunti ya Dereva wa Bolt kupitia http://partners.bolt.eu kwa kuingiza jina la mtumiaji na nenosiri.
13. **Bakshishi** – ni takrima inayotolewa na abiria kwa hiari yake juu ya nauli aliyolipa.
14. **Huduma za Usafiri** – ni huduma ya usafiri inayotolewa na Dereva kwa abiria ambaye maombi yake yamekubaliwa na Dereva kupitia programu ya Bolt.

3. **KUINGIA KWENYE MAKUBALIANO**
4. 
    1. Kabla ya kutumia huduma za Bolt, unapaswa kujisajili kwa kutoa taarifa zilizoombwa katika maombi ya usajili katika tovuti na kupakia nyaraka husika kama tunavyozitaka. Unaweza kujisajili kama mtu asilia au mtu wa kisheria. Pale utakapofanikiwa maombi ya usajili, tutakupatia akaunti yako binafsi inayofikika kupitia jina la mtumiaji na nenosiri. Kwa kubonyeza kitufe cha “Jisajili” kilichopo mwisho wa maombi ya usajili, unathibitisha na kuonesha kuwa:
    2. 
        1. kwa kufuata matendo halali, unastahili kuingia kwenye makubaliano na sisi ili kutumia jukwaa la Bolt kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Usafiri;
        2. Umejifunza kwa makini, umeelewa na unakubali kufungwa na masharti haya ya Jumla, ikiwa ni pamoja na majukumu mengine yanayojitokeza kama ilivyoanishwa katika Makubaliano;
        3. Taarifa zote ulizowasilisha kwetu za ni kweli, sahihi na kamili;
        4. utaweka Akaunti ya Dereva wa Bolt sahihi na taarifa zako zikiwa kamili muda wote;
        5. Hautaruhusu watu wengine kutumia Akaunti yako ya Dereva wa Bolt wala kuhamisha au kumkabidhi mtu mwingine;
        6. Hutatumia huduma za Bolt kwa kusudio lisiloruhusiwa au kinyume cha sheria na kuathiri utendaji sahihi wa Huduma za Bolt;
        7. Wakati wote, utafuata sheria zote na kanuni zinazotumika katika nchi unayotoa Huduma za Usafiri, ikiwemo (lakini bila ukomo) sheria zinazosimamia huduma za usafirishaji wa abiria;
    3. Unapaswa kutoa taarifa zako za kibenki pindi unapojaza taarifa za malipo wakati wa usajili. Endapo wewe ni mtu wa kisheria, unapaswa kuingiza akaunti ya benki ya kampuni. **Tunalipa ada ya malipo ya ndani ya programu kwenda akaunti ya benki uliyoitoa. Hatutakuwa na hatia kwa miamala iliyokosewa kama utakuwa umetoa taarifa za benki zisizo sahihi.**
    4. **Baada ya kutuma maombi yako ya usajili, utapokea barua pepe ikiwa na masharti ya nyongeza unayopaswa kuyatimiza ili uweze kutumia Huduma za Bolt. Masharti hayo yanaweza kukutaka kutoa taarifa ama kumbukumbu za jinai, leseni halali ya udereva, hali inayoridhisha na kiufundi ya gari lako, kuhitimu kozi ya mafunzo, umiliki wa simu inayoruhusu matumizi ya GPS na masharti mengine kama yatakavyoainishwa kwenye barua pepe husika. Kushindwa kutimiza mahitaji na masharti tajwa inaweza kupelekea kuvunjwa kwa Makubaliano na haki ya kutumia Huduma za Bolt.**
    5. Unakubali kuwa katika miji au nchi maalum Bolt Operations OÜ inaweza kukabidhi wajibu wao unaotokana na Masharti ya Jumla au Makubaliano kwa kampuni iliyopo kwenye Kundi la Makampuni ya Bolt na washirika wake. Hii inajumuisha, miongoni mwa mengine, kukabidhisha haki na wajibu wa kurejea nyaraka zinazohusu

maombi ya usajili, mafunzo, ukusanyaji wa Ada za Bolt, kutuma kwako ada stahiki, kusimamia malipo ya kimfumo, kulipia leseni ya programu ya Bolt, n.k. Taarifa zaidi kuhusu kundi la makampuni ya Bolt na washirika wake inaweza kupatikana hapa http://bolt.eu/cities.

6. Kusajili akaunti kama mtu wa kisheria (yaani, kampuni). Unachukuliwa kuwa mtu wa kisheria, kama mpokeaji wa ada amewekwa kuwa mtu wa kisheria kwenye taarifa za malipo (kama inavyopatikana kwenye Akaunti ya Dereva wa Bolt). Katika mazingira hayo, mtu wa kisheria aliyeoneshwa ndio atachukuliwa kama mtoa Huduma za Usafiri na mhusika katika masharti haya ya jumla, Makubaliano na makubaliano mengine. Mtu asilia aliyeonyeshwa wakati wa hatua za usajili ndie pekee anaweza kutoa Huduma za Usafirishaji kihalali. Mtu huyo asilia anaweza kutumia akaunti ya Dereva endapo amesoma na kukubali kuwajibika na Masharti haya ya Jumla na nyaraka nyingine ambazo ni sehemu ya Makubaliano. **MTU WA KISHERIA KATIKA TAARIFA ZA MALIPO NA MTU ASILIA ANAYETOA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI KATIKA AKAUNTI YA BOLT KWA PAMOJA NA KILA MMOJA WATAHUSIKA NA UKIUKWAJI WOWOTE WA MASHARTI HAYA YA JUMLA NA MAKUBALIANO YALIYOFANYWA NA DEREVA.**
7. Kusajili Akaunti ya Dereva wa Bolt kama kampuni ya Usafirishaji. Baada ya kukamilisha makubaliano tofauti, kampuni ya usafirishaji inaweza yenyewe kusajili akaunti kwa wafanyakazi wake na/au watoa huduma. Katika mazingira hayo, kampuni ya usafirishaji itapaswa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake na/au watoa huduma wanafuata matakwa ya Masharti ya Jumla, Makubaliano na makubaliano mengine na kukubali kutenda kadiri ya na kubanwa na masharti yake na majukumu. Kampuni ya usafirishaji na wafanyakazi na/au watoa huduma wake kwa pamoja na kila mmoja watahusika na kwa ukiukwaji wowote uliofanywa na mfanyakazi na/au mtoa huduma husika.

5. **HAKI YA KUTUMIA PROGRAMU YA BOLT NA AKAUNTI YA DEREVA WA BOLT**
6.
    1. Leseni ya kutumia programu ya Bolt na Akaunti ya Dereva wa Bolt. Kulingana na kukidhi Makubaliano haya, tunakupatia leseni ya kutumia programu ya Bolt na Akaunti ya Dereva wa Bolt. Leseni haikupi haki ya kuwapa leseni wengine au kuhamisha haki yoyote kwa watu wengine. Bila kujali yaliyosemwa hapo juu na kama imekubaliwa tofauti, makampuni ya usafirishaji yanaweza kutoa leseni ya programu ya Bolt na Akaunti ya Dereva wa Bolt kwa wanachama wao.
    2. Wakati wa kutumia programu ya Bolt na/au Akaunti ya Dereva wa Bolt hutaweza:
    3.
        1. Kutenganisha, kurejesha nyuma kihandisi, au kwa kivinginevyo kujaribu kupata chanzo cha programu ya Bolt, Akaunti ya Dereva wa Bolt au mifumo mingine ya Bolt;
        2. Kubadilisha programu ya Bolt au Akaunti ya Dereva wa Bolt kwa namna au njia yoyote au kutumia mifumo iliyobadilishwa ya programu ya Bolt au Akaunti ya Dereva wa Bolt.
        3. Kuhamisha mafaili yenye virusi, mafaili yaliyoharibika, au programu nyingine zozote zinazoweza kudhuru au kuharibu vibaya utekelezaji wa programu ya Bolt;
        4. Kujaribu kuingia bila ruhusa katikaprogramu ya Bolt, Akaunti ya Dereva wa Bolt au Huduma nyingine za Bolt.
    4. **Ili kudumisha usalama katika jukwaa la Bolt, Bolt inaweza kuomba uthibitishe**

**utambulisho wako au utambulisho wa mtu yeyote aliyeruhusiwa kufanya kwa niaba yako kuhakikisha kwamba mtu anayetumia programu ya Bolt ni yule ambaye taarifa zake zilitolewa wakati wa maombi ya usajili. Hutaweza kutoa huduma za Usafirishaji mpaka wewe au mtu aliyeruhusiwa kufanya kwa niaba yako amepitia hatua ya uthibitisho. Endapo utashindwa au mtu aliyeruhusiwa kufanya kwa niaba yako atashindwa kupitia hatua ya uthibitisho, Akaunti yako ya Dereva wa Bolt inaweza kusimamishwa au kufungwa, kulingana na mazingira husika**.

5. Leseni iliyotolewa itakoma moja kwa moja pale Makubaliano haya yatakapositishwa. Baada ya kusitishwa kwa Makubaliano haya unapaswa kuacha mara moja kutumia programu ya Bolt na Akaunti ya Dereva wa Bolt na tuna haki ya kusimamisha na kufuta Akaunti ya Dereva bila kutoa taarifa.
6. **Matumizi ya alama na nembo za Bolt. Kwa kuongeza, tunaweza kukupatia alama, nembo, vipeperushi au alama nyingine zinazowakilisha chapa ya Bolt au vinginevyo kuonesha kuwa unatumia jukwaa la Bolt. Tunakupatia leseni isiyo na kikomo, isiyogawika, isiyohamishika kutumia alama hizo na kwa ajili tu ya kuonesha kuwa unatoa Huduma za Usafirishaji kupitia jukwaa la Bolt. Baada ya kusitisha Makubaliano haya unapaswa mara moja kuondoa na kutupa alama yoyote inayoonesha chapa ya Bolt.**
7. Haki miliki zote na alama za kibiashara, ikiwemo chanzo msimbo, hifadhidata, picha nakishi na alama za picha zinamilikiwa na Bolt na kulindwa na sheria za hati miliki, alama za kibiashara na/au usiri wa kibiashara na vipengele vya makubaliano ya kimataifa. **Kutumia kwako jukwaa la Bolt au Huduma yoyote ya Bolt hakukupi haki yoyote ya umiliki wa miliki.**

7. **UTOAJI WA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**
8. 
    1. Wajibu wa Dereva. Unategemewa kutoa Huduma za Usafirishaji kulingana na Masharti ya Jumla, Makubaliano pamoja na sheria na kanuni zinazotumika katika nchi unapotoa Huduma za Usafirishaji. **Tafadhali, tambua kuwa unawajibika kwa ukiukwaji wowote wa sheria za ndani na kanuni zitakazotokea wakati wa utoaji wa Huduma za Usafirishaji.**
    2. **Unapaswa kuwa na leseni zote (ikiwemo leseni ya udereva halali), vibali, bima ya gari, bima ya fidia (kama inahitajika), usajili, vyeti na nyaraka nyinginezo zinazohitajika katika mamlaka kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Usafirishaji. Ni jukumu lako kuwa na nyaraka halali zilivyotajwa hapo juu. Bolt inahifadhi haki ya kukutaka kuwasilisha ushahidi na kuleta kwa ajili ya marejeo leseni muhimu, vibali, ruhusa, mamlaka, usajili na vyeti.**
    3. **Unahitajika kutoa Huduma za Usafirishaji kwa namna sahihi kulingana na nidhamu za kibiashara zinazotumika katika kutoa huduma na kujidhatiti kutoa huduma kwa abiria kwa maslahi ya abiria. Pamoja na hayo, unapaswa**
    4. 
        1. **Hakikisha unachukua barabara yenye gharama ya chini kwa abiria, endapo tu kama abiria mwenyewe ameomba vingine;**
        2. **Hupaswi kusimama bila ruhusa;**
        3. **hutakiwi kuwa na abiria kwenye gari zaidi ya abiria mwenyewe na abiria aliyeambatana na abiria; na**
        4. **Unapaswa kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani, kama vile, kutokufanya vitendo vinavyoweza kuathiri uendeshaji na hali ya**

**usalama barabarani, ikiwemo kushika simu mkononi mwako au kutumia simu wakati gari linatembea.**

5. **Unayo haki ya kuamua wakati wa kutoa Huduma ya Usafirishaji. Unaweza kukubali, kukataa au kuacha maombi ya Huduma ya Usafirishaji yaliyofanywa na abiria kwa utashi wako. Hata hivyo, Bolt inaweza kukusimamisha kwenye jukwaa kama unatumia jukwaa isivyo sahihi, ikiwa ni pamoja na kama kiwango cha upokeaji wako kinashuka chini ya kiwango stahiki kama ilivyowasilishwa kwako na Bolt.**
6. **Gharama unakazotumia wakati unatoa Huduma za Usafirishaji. Unawajibika kutoa na kutengeneza vifaa vyote na njia zote muhimu kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Usafirishaji kwa gharama zako mwenyewe, ikiwemo gari, simu janja, n.k. Unawajibika pia kulipa kulipa gharama zote unakazotumia wakati wa kutoa Huduma ya Usafirishaji ikiwemo, lakini bila kikomo kwa, mafuta, gharama za vifurushi kwenye simu, ada ya huduma, malipo ya gari, bima, kodi stahiki ya kampuni au kodi ya mtu, n.k. Tafadhali, kumbuka kuwa kutumia programu ya Bolt inaweza kukuletea matumizi makubwa ya vifurushi kwenye matumizi ya ya vifurushi kwenye simu yako. Hivyo, tunapendekeza uingie kwenye mpango wa vifurushi usio na kikomo au uwezo mkubwa wa matumizi ya vifurushi.**
7. Nauli. Unastahili kutoza nauli kila mara unavyokubali abiria kwenye jukwaa la Bolt na kukamilisha Huduma ya Usafirishaji kama ilivyoombwa (yaani, nauli). Nauli inakokotolewa kulingana na nauli stahiki, umbali wa safari husika kama ilivyotambuliwa na kifaa chenye GPS na muda uliotumika kumaliza safari husika. Msingi wa malipo unaweza kubadilika kulingana na mazingira ya soko la ndani. Kwa malipo ya ndani ya programu, unaweza kujadiliana nauli kwa kututumia ombi husika lililotolewa kidigitali au kwa mkono. **Kwa kuongeza, utakuwa na haki ya kutomtoza abiria nauli iliyo chini ya nauli iliyooneshwa kwenye programu ya Bolt. Hata hivyo, kumtoza abiria chini ya kiasi kinachoonekana kwenye programu ya Bolt haitapunguza ada ya Bolt.**
8. **Nauli ya awali**. Abiria ataweza kuchagua safiri inayomruhusu abiria kukubali nauli iliyowekwa kwa ajili ya Huduma ya Usafirishaji inayotolewa na wewe (yaani, nauli ya awali). Nauli ya awali inatolewa kupitia programu ya Bolt kwa abiria kabla ya kutuma ombi la safari, na kwako kabla ya kupokea ombi la safari au mwisho wa safari. Nauli inayokokotolewa kulingana na kipengele cha 4.6 itatumika badala ya Nauli ya awali kama abiria atabadilisha kituo cha mwisho wakati wa safari, na safari ikachukua muda mrefu kuliko muda uliokadiriwa kutokana na foleni au sababu nyingine, au endapo mazingira yasiyotegemewa yakaathiri safari husika (mfano, endapo safari imetumika pale ushuru unapotumika).
9. Kwenye masoko yenye programu ya malipo ya ndani, kama ukigundua kuna tatizo katika ukokotoaji wa nauli na unataka kufanya masahihisho kwenye kukokotoa nauli, unapaswa kutuma maombi katika kipengele cha ‘Marejeo ya Nauli’ kwenye programu ya Bolt. Kama maombi katika kipengele cha ‘Marejeo ya Nauli’ kwenye programu ya Bolt hayatatumwa, Bolt haitakokotoa tena Nauli au kukurudishia nauli kutokana na tatizo lililofanywa wakati wa kukokotoa Nauli. Chaguo hili halitatumika kwenye soko linalotumia malipo kwa pesa taslimu tu.
10. Bolt inaweza kurekebisha Nauli maombi maalumu yaliyomalizika, kama tukigundua kuna ukiukwaji (kama kuchukua safari ndefu au kutokusimamisha mita ya nauli ya Bolt baada ya kumaliza Huduma ya Usafirishaji) au endapo tatizo la kimfumo

linaloathiri nauli ya mwisho limejulikana. Bolt pia inaweza kupunguza au kukataa Nauli endapo kuna sababu ya kuhisi udanganyifu au kuna lalamiko kutoka kwa abiria linaloonesha ukiukwaji wako. Bolt itatumia haki yake ya kupunguza au kukataa nauli kwa njia stahiki na inayokubalika.

11. **Abiria wana chaguo la kulipa nauli kwa ajili ya Huduma za Usafirishaji kwako moja kwa moja au kupitia malipo ya ndani ya programu, katika masoko ambayo chaguo hili lipo**, kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 6 cha Masharti haya ya Jumla. **Endapo abiria amelipa nauli kwako moja kwa moja, ni wajibu wako kupokea nauli. Endapo abiria atashindwa au atagoma kulipa, Bolt itatuma notisi ya deni kwa abiria kwa niaba yako. Mamlaka haya yanatokana na uwezo wa Bolt kama wakala wa malipo na haimaanishi kuwa Bolt ina wajibu wa kufidia Nauli ambayo haijalipwa na abiria. Kama abiria ndani ya gari wameshindwa kuafikiana kulipa Nauli kwa ajili ya Huduma ya usafiri, Nauli italipwa na abiria aliyeomba Huduma ya usafiri. Kama abiria atagoma kulipa Nauli kwa kigezo cha kwamba taarifa zako sio sahihi kama zilivyotolewa kwenye programu ya Bolt, basi Bolt haitakurudishia gharama hizo.**
12. Bakshishi. **Katika baadhi ya masoko abiria anaweza kupewa nafasi ya kutoa bakshishi baada ya kupewa Huduma za usafiri.** Abiria anaweza kutoa bakshishi kwako kwa namna iliyoruhusiwa na Bolt kwenye utoaji wa bakshishi. **Bakshishi haitaathiri kiasi cha Nauli za Bolt na Bolt haitakusanya ada kwenye bakshishi iliyolipwa na abiria.** Unawajibika kutimiza wajibu wako wa kulipa kodi inayotokana na bakshishi. Tunaweza kuamua kuweka ukomo wa thamani ya bakshishi kwa busara yetu.
13. Risiti**. Kila baada Huduma za Usafirishaji kukamilika, Bolt itatengeneza na kutuma risiti kwa abiria ikiwa na taarifa baadhi ya taarifa zifuatazo: jina la kampuni la kibiashara, eneo la biashara, jina la kwanza na jina la ukoo la Dereva, picha ya Dereva, namba ya leseni ya huduma (kama inahitajika), namba ya usajili ya gari, tarehe, mwanzo na mwisho wa safari, muda na umbali, Nauli na bakshishi vilivyolipwa kwa ajili ya Huduma za Usafirishaji. Risiti ya kila Huduma za Usafirishaji inayotolewa unaweza kuipata kupitia Akaunti yako ya Dereva wa Bolt.**
14. **Endapo kuna malipo ya pesa taslimu, utawajibika kukusanya ada zote za huduma za jukwaa kwa niaba ya Bolt kutoka kwa abiria. Huduma ya jukwaa ni tozo iliyowekwa na Bolt kwa ajili ya matumizi ya abiria ya programu ya Bolt na iko tofauti na Nauli.** Ada ya huduma ya jukwaa inayokusanywa na dereva itarudishwa kwa Bolt kwa muda uliopangwa, kulingana na ratiba za malipo ya programu ya Bolt au kama itakavyowasilishwa kwako na Bolt.
15. Gharama za kughairi na gharama za kusubiri. **Abiria anaweza kughairi ombi lake la Huduma za Usafirishaji ambalo Dereva amelikubali kwenye programu ya Bolt. Katika baadhi ya masoko, Madereva wanaweza kustahili kupata Nauli ya kughairi Huduma ya Usafirishaji (gharama ya kughairi)** katika tukio ambalo abiria ameghairi ombi lililopokelewa la Huduma za Usafirishaji baada ya muda fulani uliotambuliwa na programu ya Bolt.
16. **Endapo wakati wa kutoa Huduma za Usafirishaji, abiria au abiria wenzie wataharibu gari kwa uzembe au samani zake (ikiwemo kwa kutia doa au kuchafua gari au kusababisha gari kuwa na harufu mbaya) utakuwa na haki ya kumwomba abiria kulipa faini ya hadi EUR 50 na kuomba fidia kwa**

**madhara yoyote yanayozidi faini hiyo.  Kama abiria hatokubali kulipa faini na/au kufidia uharibifu, unapaswa kutujulisha na tutajaribu kukusanya faini na/au gharama husika kwa niaba yako kutoka kwa abiria. Hata hivyo, kumbuka kuwa hatutakuwa na hatia kwa ajili ya madhara yoyote ya moja kwa moja au madhara mengine yanayohusiana na usafirishaji au matengenezo ya gari yaliyosababishwa na abiria.**

17. Wajibu wako wa kodi**. Unaridhia kuwa unawajibika kutimiza wajibu wako wa kodi unaotokana na sheria zinazotumika kwenye utoaji wa Huduma za Usafirishaji, ikiwemo**
18.
    1. **Kulipa kodi ya mapato, kodi ya mfuko wa hifadhi ya jamii, na kodi nyingine zinazohusika; na**
    2. Kutimiza majukumu yote ya mfanyakazi na usajili wa kodi kwa ajili ya ukokotoaji wa taarifa za kifedha na uhamishaji pesa unaotumika katika nchi husika kulingana na matakwa ya sheria husika. **Ikitokea Mamlaka ya Kodi italeta maombi halali kwetu kupata taarifa kuhusu shughuli zako, tunaweza kuzitoa kwa Mamlaka ya Kodi taarifa za shughuli zako kadri ya matakwa ya kisheria.** Kwa kuongeza, ni jukumu lako kufuata kanuni zote za kodi zinazoweza kutumika kuhusiana na utoaji wa Huduma za Usafirishaji.  Unakubalia kuifidia Bolt ada zote za serikali, madai,  malipo, faini au wajibu mwingine wowote wa kikodi ambao Bolt itaingia kutokana na majukumu yanayokana na kanuni za kodi zinazotumika ambayo umeshindwa kukidhi (ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya mapato  na kodi ya mfuko wa hifadhi ya jamii).
19. Kibali cha Dereva kutoa ankara. Bolt ina haki ya kutoa ankara kwa niaba yako kwa abiria ili kukufidia kwa Nauli yoyote, adhabu za kimkataba au ada nyingine zilizotumiwa na abiria. Katika masoko ambapo Bolt inatoa ankara, ankara hiyo utaipata kwako kupitia Akaunti ya Dereva wa Bolt.

9. **ADA ZA BOLT**
10.
    1. **Ili kutumia Huduma za Bolt, unahitajika kulipa ada (yaani, Ada ya Bolt au Tozo ya Bolt). Tozo ya Bolt inalipwa kutokana na nauli kwa kila oda ya Huduma za Usafirishaji iliyomalizika. Kiasi cha Tozo ya Bolt kitajulishwa kwako kupitia barua pepe, programu ya Bolt, Akaunti ya Dereva wa Bolt au njia nyingine wezeshi.** Tafadhali kumbuka kuwa Tozo ya Bolt inayotozwa inaweza kubadilika mara kwa mara kwa kuangalia kanuni za mabadiliko ya utozaji tozo ambayo yanaangalia: Usawa wa usambazaji na uhitaji wa Huduma za Usafirishaji, Sifa za usafiri ulioombwa; na Masharti ya kampeni yoyote. **Tozo ya Bolt ni 18% ya Nauli.**
    2. **Unapaswa kulipa Ada ya Bolt na ada nyingine unazodaiwa kwa mwezi uliopita angalau kabla ya tarehe 15 ya mwezi unaofuata. Tunaweza kuchagua kuweka kikomo kwenye kiwango cha juu cha ada unayodaiwa kutoka kwako kwenda kwa Bolt kwa wakati muafaka ili kupunguza madhara ya kutokulipa**. Endapo utachelewa kulipa ada ya Bolt, utawajibika kulipa faini ya kuchelewesha malipo kwa kiwango cha 0.04% (asilimia sifuri nukta sifuri nne) ya kiasi ambacho hakijalipwa kwa kila siku. Utawajibika pia kufidia gharama zote tutakazokuwa tumeingia, zinahusiana na shughuli za ukusanyaji wa madeni.

11. **MALIPO YA NDANI YA PROGRAMU**
12.

1. Tunaweza kuwaruhusu abiria kulipia Huduma za usafiri kwa njia ya kadi, malipo ya ubebaji, na njia nyingine za malipo (Bolt-Biashara, n.k) moja kwa moja kwenye programu ya Bolt (yaani, malipo ya ya ndani ya programu). Unaturuhusu sisi kama wakala wako wa kibiashara kupokea Nauli au ada nyingine zilizolipwa na abiria kupitia Malipo ya ndani ya programu na kutuma pesa husika kwako. Malipo yoyote yaliyofanywa na abiria kupitia Malipo ya ndani ya programu yatakamilika pale malipo yatakapofanyika.
2. **Hutaweza kukataa malipo ya abiria kupitia malipo ya ndani ya programu, au kumshawishi abiria kutokutumia Malipo ya ndani ya programu.** Endapo utagoma kupokea Malipo ya ndani ya programu bila sababu ya msingi, tutakuwa na mamlaka ya kukutoza faini ya kimkataba ya kiasi cha EURO 15 kwa kila ulipokataa na/au kuzuia haki ya Huduma za Bolt endapo tabia itajirudia.
3. **Bolt inayo haki kusambaza msimbo wa matangazo kwa abiria kwa ridhaa yetu kulingana na vigezo vya matangazo. Utahitajika kukubali matumizi ya msimbo wa matangazo pale tu abiria ameomba msimbo kwenye programu.** Endapo matumizi ya msimbo wa matangazo yatahisiwa kuwa na udanganyifu, haramu, na kutumiwa na Dereva kinyume cha Vigezo na Masharti yetu kuhusiana na matumizi ya msimbo wa matangazo, Msimbo wa matangazo unaweza kuzuiliwa na kiasi kilichobaki hakitarudishwa na Bolt kwa Dereva.
4. **Endapo kuna nafasi na abiria akachagua kukupatia bakshishi moja kwa moja katika Mfumo wa Bolt, bakshishi itakusanywa na Bolt kwa niaba yako pamoja na Nauli na ada nyingine zilizolipwa na abiria kupitia Malipo ya Kimfumo.** Endapo malipo ya bakshishi yanahisiwa kuwa ya kidanganyifu, haramu, kwa namna yoyote nje ya nyongeza inayohusiana na huduma iliyotolewa au kutumiwa na Dereva ni kinyume na Vigezo na Masharti basi Bolt inaweza kushikilia malipo hayo.
5. **Unaweza kurejea tarifa ya Malipo ya ndani ya programu kwenye Akaunti ya Dereva wa Bolt au kwenye programu.Kumbukumbu zitaonesha kiasi ambacho kilipokelewa kwenye malipo ya ndani ya programu kwa wiki iliyopita pamoja na kiasi kilichozuiliwa cha Ada ya Bolt.** Unapaswa kutujulisha mazingira yoyote yanayoathiri wajibu wetu wa kukusanya na kurejesha Nauli iliyolipwa kwa njia ya Malipo ya ndani ya programu.
6. **Hatutahusika kukulipa Nauli unayodai kutoka kwa abiria kama Malipo ya ndani ya programu yameshindikana kwa sababu malipo aliyofanya abiria kwa kadi yamefutwa au malipo mengine yameshindikana au yamekwama kwa sababu nyingine zozote. Katika mazingira hayo, tutakusaidia kwa kuomba Nauli unayodai kutoka kwa abiria na tutairudisha kwako pale tu abiria atakapotoa malipo hayo**.
7. **Kabla ya kutoa Huduma ya Usafirishaji, unapaswa kuthibitisha kuwa huduma inatolewa kwa abiria sahihi au abiria amethibitisha bayana kwamba ameruhusu abiria wengine kutumia Akaunti yake kusafiria. Kama ukifanya makosa ya kumtambua abiria, na Malipo ya ndani ya programu yakakatwa kutoka kwa mtu ambaye hajapewa huduma au hajaruhusu Huduma ya Usafirishaji itolewe kwa abiria wengine, tutamrudishia mtu huyo Nauli. Katika mazingira hayo, hautakuwa na haki ya kupokea Nauli kutoka kwetu.** Pia, kwa kila Malipo ya kimakosa kwenye programu, tutakuwa tunakutoza faini ya kimkataba hadi EURO 10.
8. Tafadhali Kumbuka kuwa tutakata Nauli yoyote au bakshisi iliyolipwa kwa njia ya

Malipo ya ndani ya programu dhidi ya kiasi unachopaswa kutulipa (yaani, Ada za Bolt, na faini za kimkataba). Tunatunza haki ya kutimiza wajibu wa madeni ya kifedha kwa kampuni yoyote kwenye kundi la Makampuni ya Bolt, na kwa namna hiyo tutakuwa na haki ya kuwasilisha madai dhidi yako. Tunaweza kupunguza madeni yako ya kifedha dhidi ya madeni ya kifedha unayoweza kuwa nayo dhidi yetu.

9. **Nauli na malipo mengine unayodai kulingana na kipengele cha 6.1 hapo juu yatatumwa kwako mara kwa mara, kwa kawaida mara moja kila wiki au muda mwingine kadri utakavyojulishwa mapema na Bolt.** Tutatuma fedha zote stahiki kulingana na kipengele cha 6.1 hapo juu, ambazo tumekusanya kwa niaba yako kwenda akaunti ya benki uliyoiweka kwenye akaunti yako ya Dereva. **Bolt inaweza kuamua, kwa hiari yake, kuhamisha fedha kwa awamu nje ya muda ulioainishwa kulingana na ukomo na masharti yaliyotolewa na Bolt.**
10. Kama hatutaweza kuhamisha Ada au bakshishi unazodai kwa sababu ya kutokutoa taarifa zako za akaunti ya benki kwenye akaunti ya Dereva au kama taarifa zako za akaunti ya benki haziko sahihi, tunaweza kuzuia malipo hayo kwa siku 180. Endapo hautatujulisha taarifa zako sahihi za akaunti ya benki ndani ya siku 180 tangu tarehe haki yako ya kudai malipo ilipoanza, madai yako kuhusu malipo ya Nauli au bakshishi kutokuhamishiwa kwako yatafikia ukomo.

13. **MSAADA KWA WATEJA**

14.

1. Tunawapa Madereva msaada kwa wateja kuhusu matumizi ya Huduma za Bolt. Tuna haki ya kuacha kutoa huduma za msaada kwa wateja endapo utachelewesha malipo yoyote kwa Bolt zaidi ya siku 5 (tano) za siku za kalenda.

15. **MAKADIRIO NA SHUGHULI**

16.

1. Ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na kutoa uhakika kwa abiria, unakubali kuwa abiria watakupa makadirio na kuacha mrejesho kuhusu ubora wa Huduma za usafiri ulizotoa. Wastani wa makadirio yako yataunganishwa kwenye akaunti yako ya Dereva na yatakuwepo kwa abiria kwenye programu ya Bolt. Kama tukigundua kuwa makadirio au mrejesho hayajatolewa kwa nia njema, makadirio au mrejesho huo hautatumika kukokotoa makadirio yako.
2. Kwa kuongezea, kwenye makadirio tunapima hatua yako ya utendaji na kukupatia alama ya utendaji, ambayo inatokana na shughuli zako kuhusu kupokea, kukataa, kutokuwajibika na kumaliza maombi ya Huduma za Usafirishaji.
3. **Ili kutoa huduma za uhakika kwa abiria, tunaweza kuweka viwango vya chini vya wastani na alama za chini za utendaji ambazo Madereva wanapaswa kuzifikia na kutunza. Endapo, baada ya ujumbe kutoka kwetu, hujaweza kuongeza wastani wako wa makadirio au alama za utendaji wa kiwango cha chini kinachotakiwa ndani ya muda uliotolewa, akaunti yako ya Dereva itasimamishwa kwa muda au moja kwa moja. Tunaweza kurejea kusimamisha akaunti yako kama iliathiriwa na mazingira yoyote ya nje au endapo imegundulika kuwa sitisho hilo lilisababishwa na tatizo la kimfumo au makadirio yasiyo ya kweli.**

17. **MAPITIO YA SOKO NA KAMPENI**

18.

1. Mapitio ya Soko. Tunaweza kukutumia kupitia programu ya Bolt, Akaunti ya Dereva wa Bolt, ujumbe mfupi, barua pepe au njia nyingine, mapitio ya soko, ili kukuza

uelewa wako kuhusu ni wakati gani uhitaji wa abiria unakuwa mkubwa. Mapitio hayo ya soko ni mapendekezo tu na hayatengenezi wajibu wowote kwako. Sababu makadirio kwenye mapitio ya soko yanategemea takwimu zilizopita, hatuwezi kutoa uhakika kuwa hali ya soko halisi itakuwa sawa na makadirio yaliyotolewa kwenye mapitio ya soko.

2. Kampeni zinazoahidi kipato cha chini. **Tunaweza kutoa kampeni, ambazo tutakuhakikisha kipato cha chini kama ukitoa Huduma za Usafirishaji ndani ya muda husika. Kama kiwango cha chini tajwa hutaweza kukifikia, tutafidia pengo lililobaki. Mahitaji ya msingi na masharti yatatumwa kupitia programu yaBolt, Akaunti ya Dereva wa Bolt, ujumbe mfupi, barua pepe au njia nyingine. Tunayo mamlaka ya kuamua kama, lini na kwa Madereva gani tutawapa kampeni hiyo. Kama tutakuwa na sababu ya msingi kuhisi unajihusisha na kazi za kilaghai, tunaweza kuzuia Nauli yako hadi hisia za ulaghai zitakapofutwa.**

19. **UHUSIANO KATI YAKO, SISI NA WASAFIRI**

20.

1. **Unatambua na kukubali kuwa tunatoa taarifa ya huduma za jamii na hatutoi Huduma za Usafirishaji. Kwa kutoa jukwaa la Bolt na Huduma za Bolt, tunasimama kama eneo la soko linalounganisha abiria na Madereva ili kusaidia kuzunguka ndani ya miji kwa ufanisi. Unatambua kuwa unatoa Huduma za Usafirishaji kadri ya mkataba wa ubebaji abiria na unatoa Huduma za Usafirishaji ukiwa huru au kupitia kampuni kama shughuli ya kiuchumi na kiutaalamu. Bolt, kama waendeshaji wa programu ya Bolt itasimama kama wakala wa kibiashara wa Madereva katika kusaidia kukamilika kwa mikataba kati ya Dereva na abiria, na hivyo, pamoja na vitu vingine, kupokea malipo kutoka kwa abiria na kutuma malipo hayo kwa Dereva.**
2. Unatambua kuwa hakuna mkataba wa ajira na hakuna mahusiano ya ajira yaliyoanzishwa au yatayoanzishwa baina yako na sisi. Unatambua pia kuwa hakuna biashara ya pamoja au ushirikiano baina yetu na wewe. Huwezi kusimama kama mfanyakazi, wakala au mwakilishi wetu wala kuingia kwenye mkataba wowote kwa niaba yetu. Kama kwa mtazamo wa sheria husika au kivingine, utachukuliwa kuwa mfanyakazi wetu, unakubali kutokuwa na madai yoyote dhidi yetu yatayoibuka kama matokeo ya mahusiano ya kikazi kutokana na mtazamo huo wa sheria.
3. Huwezi kuhamisha haki zako na wajibu zinazotokana na Masharti ya Jumla au Makubaliano kwa mtu mwingine.

21. **UCHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI, UFIKIAJI WA TAARIFA**

22.

1. Taarifa zako binafsi zitachakatwa kulingana na Notisi ya Usiri, inayopatikana [https://bolt.eu/en-ke/privacy/privacy-for-drivers/?category=rides](https://bolt.eu/en-ke/privacy/privacy-for-drivers/?category=rides) .
2. Bolt inaweza kufikia taarifa zako binafsi na taarifa nyingine zitolewazo au zinazotengenezwa kulingana na matumizi yako ya Huduma za Bolt. Bolt itachukua hatua stahiki kuhakikisha Usiri wa taarifa hizo na kufuata Sera za Usiri zilizopo na sheria pale taarifa hizo zitakuwa na taarifa binafsi. Isipokuwa pale itakapotolewa tofauti na Sera za Usiri na sheria, Bolt inatunza ufikikaji wa taarifa hizo pia hata baada ya Makubaliano kati yako na Bolt kusitishwa.
3. Unaweza kufikia taarifa zako binafsi na taarifa nyingine ulizozitoa au zilizotengenezwa kulingana na matumizi yako ya Huduma za Bolt kadri

zitakavyotolewa kwako kupitia Akaunti yako ya Dereva wa Bolt kwenye programu ya Bolt. Unapaswa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha usiri wa taarifa hizo na kufuata Sera za Usiri zilizopo na sheria pale ambapo taarifa hizo zinakuwa na taarifa binafsi za abiria.

23. **DHIMA**

24.

1. Jukwaa la Bolt linatolewa kwa kigezo cha 'kama ilivyo' na 'kama inavyopatikana". Hatuwasilisha, kuthibitisha au kuhakikisha kuwa kufikia jukwaa la Bolt hakutaingiliwa au hakuna makosa. **Kwa sababu matumizi ya jukwaa la Bolt kuomba huduma za usafirishaji unategemea tabia za abiria, hatuthibitishi kuwa matumizi ya jukwaa la Bolt kutapelekea maombi yoyote ya Huduma za Usafirishaji.**
2. **Kwa kiwango cha juu kilichoruhusiwa na sheria iliyopo, sio Bolt wala wawakilishi wake, wakurugenzi na wafanyakazi watahusika kwa hasara yoyote au madhara utakayopata kwa ajili ya matumizi ya Huduma za Bolt, ikiwa ni pamoja na ila sio kikomo;**
3.
    1. **Uharibifu wa moja kwa moja au wa mbali wa mali au hasara ya pesa;**
    2. **Kukosa faida au akiba tarajiwa;**
    3. **Kupoteza biashara, mikataba, mawasiliano, uaminifu, heshima na hasara yoyote inayoweza kutokea kutokana na mwingiliano wa biashara;**
    4. **Kupoteza au kuwa na taarifa zisizosahihi, na**
    5. **Aina nyingine yoyote ya hasara au madhara.**
4. Wajibu wetu wa kifedha unaohusiana na uvunjifu wa Vigezo vya Jumla au Makubaliano utakuwa na kikomo cha EURO 500. Utakuwa na haki ya kudai fidia pale tutakapokuwa tumevunja Masharti ya Jumla au Makubaliano kwa makusudi.
5. **Hatutawajibika kwa matendo au yasiyo matendo ya abiria au abiria wenzake na hatutawajibika kwa hasara au madhara utakayopata au gari lako kutokana na matendo au kutokufanya kwa abiria au abiria wenzake.**
6. Utawajibika kwa ukiukwaji wa Mashsarti haya ya Jumla, Makubaliano au sheria au kanuni nyingine na unapaswa kuacha na kurekebisha ukiukwaji huo mara baada ya kupokea wito kutoka kwetu au mamlaka yoyote ya serikali. Utawajibika kutufidia kwa hasara yoyote, iwe ya moja kwa moja au hasara ya mbali/hasara/kupoteza faida/gharama/ faini tutakayopata kutokana na uvunjifu wako wa Vigezo vya Jumla, Makubaliano na sheria na kanuni husika. **Kama abiria akileta malalamiko yoyote kwetu yanayohusiana na utoaji wako wa Huduma za Usafirishaji, utawajibika kufidia hasara hiyo kwetu ndani ya siku 7 (saba) baada ya kupokea ombi hilo kutoka kwetu. Endapo tunastahili kuleta madai yoyote dhidi yako, utatakiwa kutufidia kwenye gharama zozote za kisheria zinazohusiana na kufanya tathmini ya madhara na uwasilishwaji wa madai yanayohusu fidia ya hasara hiyo.**

25. **MUDA, KUSIMAMISHWA NA KUSITISHWA**

26.

1. **Masharti yaliyoelezwa wazi kwenye hivi Masharti haya ya Jumla yataanzaa rasmi baada ya kutuma maombi ya usajili. Makubaliano na vigezo vingine vitaanza rasmi baada ya nyaraka husika au taarifa kuwa imekufikia na ukaanza au kuendelea kutoa Huduma za Usafirishaji kwenye jukwaa la Bolt.**

2. **Unaweza kusitisha Makubaliano muda wowote kwa kutoa taarifa Bolt ya angalau siku 7 (saba), baada ya hapo haki yako ya kutumia jukwaa la Bolt na Huduma za Bolt itasitishwa. Bolt inaweza kusitisha Makubaliano muda wowote kwa sababu yoyote kwa hiari yao kwa kutoa taarifa kwako angalau siku 3 (tatu) kabla.**
3. **Bolt ina haki ya kusitisha Makubaliano mara moja na kufungia kwenye jukwaa la Bolt bila kukupa taarifa ya awali endapo utakiuka Mashartiya Jumla au Makubaliano, sheria na kanuni zilizopo, kuidharau Bolt, au kuisababishia madhara chapa ya Bolt, hadhi au biashara kadri itakavyotambuliwa na Bolt kwa hiari yake. Kwa mazingira yaliyotajwa, kwa hiari yetu, tunaweza kukuzuia kusajili Akaunti mpya ya Dereva.**
4. **Pia tunaweza kukusimamisha (kukuzuia) kuingia kwenye jukwaa la Bolt na Akaunti ya Dereva wa Bolt kwa kipindi cha uchunguzi, kama tutahisi kuna uvunjifu wa Makubaliano au shughuli haramu kwa upande wako. Zuio hilo litaondolewa baada ya uchunguzi kuthibitisha kutokuwepo kwa tuhuma huo.**
5. Tunalenga kutoa huduma bora sana kwa abiria wote hivyo kufuatilia shughuli za Madereva kwenye jukwaa la Bolt. Kama ukishindwa kukidhi matakwa ya chini ya huduma, ikiwemo makadirio ya chini na alama za shughuli, tutakuwa na haki ya kuvunja mara moja Makubaliano bila kukupa notisi yoyote ya awali.

27. **MAREKEBISHO**
28.
    1. **Bolt inatunza haki ya kurekebisha Masharti haya ya Jumla muda wowote kwa kupakia toleo lillorudiwa kwenye tovuti yake ya** ([http://bolt.eu/legal/](http://bolt.eu/legal/)) na kukujulisha (mfano, kwa barua pepe, programu ya Bolt au Akaunti ya Dereva wa Bolt) endapo, kwa maoni busara ya Bolt, marekebisho hayo ni muhimu.
    2. **Bolt itatoa notisi ya awali ya siku 15 (kumi na tano) (mfano, kwa barua pepe, programu ya Bolt au Akaunti ya Dereva wa Bolt) kuhusu marekebisho yanayoathiri haki za Watumiaji wa Biashara Wanaofanya katika Nchi mwanachama,** isipokuwa**;**
    3.
        1. **Bolt ina wajibu wa kisheria au kikanuni kufanya marekebisho ya Masharti ya Jumla katika njia bila kujali kipindi cha utoaji wa notisi;**
        2. Marekebisho ya haraka yanatakiwa kutatua hatari isiyotarajiwa au hatari ya karibu inayohusiana na afya, usalama au hatari za usalama wa kimtandao, au kulinda Huduma za Bolt, Wasafiri au Madereva dhidi ya ulaghai, programu hatarishi, barua taka au uvinjifu wa tarifa;
        3. Umechagua kupoteza kipindi cha notisi ya awali (mfano, umeendela kutumia Huduma za Bolt baada ya kupokea notisi ya marekebisho); au
        4. **Katika maoni ya busara ya Bolt, marekebisho yana faida kwa Madereva na hayahitaji marekebisho ya kiufundi kutoka kwao.**
    4. **Kama haukubaliani na marekebisho ya Vigezo vya Jumla au masharti mengine ya Makubaliano, una haki ya kusitisha Makubaliano kwa kutokuendelea kutumia Huduma za Bolt na kutoa notisi ya kusitisha kwa Bolt.** Kusitisha kwa Makubaliano kutaanza rasmi siku husika ya marekebisho yaliyopendekezwa, labda itolewe tofauti katika notisi yako ya kusitisha. Matumizi yako ya Huduma za Bolt kabla na baada ya tarehe husika ya marekebisho yataunda ridhaa yako kubanwa na Masharti ya Jumla au Makubaliano, kama yalioyorekebishwa.

29. **SHERIA INAYOHUSIKA NA MAMLAKA YA MAHAKAMA**
30.
    1. **Masharti haya ya Jumla na Makubaliano vitasimamiwa na kutafsiriwa na kutekelezwa kulingana na sheria za Jamhuri ya Kenya. Kama kuna mgogoro unaotokana na Makubalino ya Jumla au Makubaliano haujatatuliwa kwa majadiliano, mgogoro huo utatatuliwa na mahakama yenye mamlaka ndani ya Kenya.**

31. **NOTISI**
32.
    1. **Unapaswa kutujulisha mara moja kwa mabadiliko yoyote ya taarifa zako za mawasiliano.**
    2. Notisi yoyote inayopaswa kutolewa chini ya Marekebisho ya Jumla na Makubaliano itatolewa kwa ukamilifu kama;
    3.
        1. Itapelekwa binafsi;
        2. Imetumwa na msafirisha mizigo ikiwa na ushuhuda wa kupokea;
        3. Imetumwa kwa anuani iliyosajiliwa;
        4. Imetumwa kwa barua pepe; au
        5. Inapatikana kupitia programu ya Bolt au Akaunti ya Dereva wa Bolt.
    4. Notisi yoyote iliyotumwa au kupelekwa kulingana na kipengele cha 16.2 itachukuliwa kuwa imepokelewa:
    5.
        1. Kama imepokelewa binafsi, wakati wa kuipeleka kwa mtu;
        2. Kama itapelekwa na msafirisha mizigo, kwa tarehe ambayo msafirisha mizigo aliinakiri kama tarehe ya kupokelewa notisi na mhusika;
        3. Kama imetumwa kwa anuani iliyosajiliwa, siku ya 10 baada ya kukabidhi nyaraka katika ofisi ya posta kwa ajili ya kupelekwa;
        4. Kama imetolewa kupitia programu ya Bolt au Akaunti ya Dereva wa Bolt, au
        5. Kama imetumwa kwa barua pepe, siku ambayo aliyepokea barua pepe hiyo amekiri kuipokea au siku ya 2 (pili) kutokea siku ya kutumwa kwa barua pepe endapo mtumaji hajapokea notisi ya tatizo (ikimtaarifu kuwa barua pepe haikufika kwa mhusika) na ametumwa barua pepe tena siku iliyofuata ya kalenda na haijapokelewa kwa sababu ya kosa kama hilo.

33. **VIPENGELE VYA MWISHO**

**Kama kipengele chochote katika Masharti ya Jumla hakiwezi kutekelezeka, wahusika wanaweza kukibadilisha kipengele hicho kwa kipengele kinachotekezeka kinachoendana na dhima na lengo la kiuchumi.**